

# HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA-MIKINDANI



## TANGAZO LA ZABUNI YA HUDUMA YA ULINZI WA SILAHA (BUNDUKI) KWENYE MAENEKO YA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI

25/05/2017

ZABUNI NA.LGA/085/2017/2018/NC/02

Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani inakaribisha maombi kwa makampuni mbalimbali yenye sifa ya kufanya kazi za ulinzi wa kutumia silaha za moto (bunduki) kwenye malindo ya Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

### MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

1. Nyaraka za maombi ya zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya zabuni ya shilingi laki moja (100,000/=) tu. Ada hiyo haitarejeshwa (Non refundable).
2. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani ya mwombaji na ataje kiasi atakacholipwa na Manispaa kwa mwezi ikiwa ni gharama za ulinzi wa silaha (bunduki) kwenye maeneo husika ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani..
3. Mwombaji anatakiwa awe na leseni hai ya huduma ya ulinzi iliyosajiliwa na mamlaka husika, awe na uthibitisho wa uzoefu wa kazi husika na uthibitisho wa uwepo wa stakabadhi za kielektroniki.
4. Maombi(halisi na nakala mbili) yafungwe kwenye bahasha ya khaki (A4) yenye lakiri na itumwe kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kwa anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,  
Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani  
S. L. P. 92  
MTWARA**

5. Kabrasha la maombi ya zabuni linapatikana katika ofisi ya Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, kuanzia saa 1.30 asubuhi mpaka saa 9.30 kwa siku za kazi (Jumatatu - Ijumaa).

Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 16/06/2017saa nne (4.00) asubuhi. Waombaji au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni katika ukumbi wa mikutano wa Manispaa.

  
**(SAMBWE P. SIJABAJE)  
KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA  
MTWARA-MIKINDANI**

# HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA-MIKINDANI



## TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NAMBA: LGA/085/2017/2018/NC/03

### ZABUNI YA UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO YA MAEGESHO YA MAGARI KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA MIKINDANI

#### MAOMBI YA ZABUNI

Date: [25/05/2017]

1. Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani inakusudia kutumia wakala kwa ajili ya kukusanya mapato ya maegesho kwa kipindi cha kuanzia Julai 1, 2017 mpaka Juni 30,2018
2. Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyoajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hiyo kutuma maombi yao kwa zabuni hii kuanzia tarehe ya tangazo.
3. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-
  - i) Nyaraka za zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya zabuni ya Tzs.50,000.00 ambayo haitarejeshwa, mwombaji atatembelea maeneo ya kukusanya mapato kabla ya kuchukua nyaraka ya zabuni.
  - ii) Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aoneshe mahali ofisi yake ilipo au anapoweza kupatikana (physical address)
  - iii) Mwombaji atakusanya mapato ya maegesho kwa kutumia mashine za kielektroniki kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa kwenye sheria ndogo za Halmashauri.
  - iv) Mwombaji anatakiwa kutaja kiasi atakacholipa Halmashauri kutokana na makusanyo atakayowasilisha.
  - v) Zingatia kuwa form ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney) katika zabuni hii.
  - vi) Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani na ambaye hajashtakiwa kwa ukiukwaji wa kazi za ukusanyaji wa mapato.Mtumishi wa Manispaa hausiki na maombi haya.
4. Mwombaji athibitishe uwezo wake wa kifedha kwa kuweka dhamana ya utendaji (performance bond) ya Tzs.Milioni tano (5,000,000.00) na ilipwe baada ya kusaini mkataba.
5. Mwombaji awasilishe zabuni Original na nakala mbili.

6. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, Original au Copy, Anuani ya Mkurugenzi bila kuwekwa alama yoyote.
7. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.
8. Makabrasha ya zabuni yanapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kanzia saa 1:30 Asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri kwa siku za kazi.
9. Mwisho wa kupokea zabuni ni saa nne (4) kamili asubuhi (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe 16/05/2017 na maombi yapelekwe katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani makao makuu kwa :-

**Katibu wa bodi ya zabuni.**

**S.L.P 92**

**Mtwara**

10. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo.
11. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitafunguliwa.

  
**Sambwe P. Sijabaje**

**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA  
MTWARA -MIKINDANI**

MKURUGENZI WA MANISPAA  
MTWARA - MIKINDANI  
S. L. P. 92  
MTWARA